HATIMA YA

WALIOFARIKI

BILA KUPOKEA

INJILI

Written by:
J. Michael Feazell

Haki ya kunakili. © 2000 Grace Communion International

Translated into Kiswahili by:
Francis Wanyoike

Nairobi GCI Shalom Congregation

nyoikefg@gmail.com

Hakuna Jina Lingine

Katika hali nyingine, Wakristo wanaamini kuwa kupitia kwa mwana wa Mungu vitu vyote viliumbwa (Wakolosai 1:16), kupitia neno lake mwana wa Mungu kila kitu kulipata kuumbwa (Waebrania 1:3), na kuwa kupitia kuzaliwa kama binadamu, kufa na ufufuo wa mwana kila kitu kinapata upatanisho na Mungu (Wakolosai :20). Lakini kwa hali nyingine wengi wanayo mawazo kuwa damu ya Yesu Kristo haiwezi patanisha wanadamu wanaokufa kabla ya kuja kwenye imani.

Kabla ya kuanza, ni vema tuelewe dhahiri maneno ya Biblia kwamba ni kupitia tu kwa Yesu Kristo pekee wokovu unapatikana. (Kitabu cha Mitume 4:12).

Dini za wanadamu hazileti wokovu. Ni katika nafsi tatu za Uungu – Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu anayeumba, anayetuokoa, kututunza na anayetawala vyote – je kuna msamaha wa dhambi, uponyaji wa fikra, urejesho na hata maisha ya milele.

Swala linaloshughulikiwa kwenye maelezo hayo ni kama Biblia inasema kuwa mtu lazima amkiri Kristo kabla yeye kufa au atakuwa amepoteza uzima wa milele moja kwa moja.

Tajiri na Lazaro:

Tuanzie kwa kuangalia fungu mojawapo ya mafungu mawili ambayo wakati mwingine yanatafsiriwa kumaanisha kuwa yeyote afaye bila kumkiri atakuwa amepotea moja kwa moja. Ni mfano wa Lazaro na tajiri, ambapo Abrahamu anamweleza tajiri upo ufa mkubwa unaotenganisha walio jehanamu na walio pamoja na Abrahamu.

Mfano huu unapatikana katika kitabu cha Luka 16:19-31; kabla ya kuanza mfano huu, turejee nyuma kidogo ili tuone ni nani Yesu alikuwa anaongea naye alipotoa mfano huu na nini kilichompelekea kuutoa mfano huo. Katika fungu la 14, tunasoma yafuatayo: “Basi mafarisayo, ambao wenyewe ni wapenda fedha, waliyasikia hayo yote, wakamdhihaki”.

Yesu alikuwa anaongea na kundi la mafarisayo, na Luka angependa wanaosoma mafungu haya wajue kuhusu mafarisayo hao ni kuwa wanapenda fedha. Sasa tunapata maelezo ya kina ya maelezo haya. Mafarisayo ambao walikuwa ni wapenda fedha walikuwa wanamdhihaki Yesu kwa sababu ya yale aliyokuwa anayasema.

Inabidi turudi sura ya kumi na tano, fungu la kwanza, ili kuelewa tukio kamili. Hapa tunasoma “Basi watoza ushuru wote na wenye dhambi walikuwa wakimkaribia wamsikilize”.

Na Yesu akaendelea kuwapa mifano mingine mitatu kwa mfurulizo: mchungaji anayesherehekea kumpata kondoo wake aliyepotea; mwanamke anayesherehekea kupata sarafu yake iliyokuwa imepotea na baba anayesherehekea kumpata mwanae mpotevu. Yesu anatoa hii mifano mitatu hasa kwa kuwajibu mafarisayo na waandishi waliokuwa wanakerwa na kitendo chake cha kuwakaribisha wenye dhambi na hata kushiriki chakula pamoja nao.

Mifano hii inawaonyesha wazi wazi mafarisayo na waandishi neema ya Mungu ilivyo kuwa kwa wenye dhambi.

Yesu alitaka wajue kuwa “Nawaambia vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atumbuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja na kutubu” Msisitizo unaowekwa unawalenda mafarisayo na waandishi; ambao walipenda kujionyesha kama watakatifu na ambao hawakuwa na umuhimu wa kutubu. Yesu (akijua kuwa walikuwa waovu) anawaambia mbingu hazifurahishwi na mienendo yao.

Mungu na fedha:

Endapo mifano hiyo miwili iliwaudhi mafarisayo na wandishi, mfano wa tatu utakuwa uliwakera zaidi, ni kuhusu baba aliyefurahi kumpata wanae aliyekuwa amepotea, anajulikana kama mwana mpotevu. Katika mfano huu baba anaonyesha pendo la pekee na msamaha usio na masharti kwa mwana aliyemdharirisha, aliyepoteza nusu ya mali ya familia, na zaidi ya yote kupoteza heshima ya familia. Ni kashfa ambayo iliiharibia sifa, heshima na ustahifu familia. Yesu alipomaliza kutoa mfano huu aligeukia wanafunzi wake na kuwapa mfano mwingine (Luka 16:1). Na bado mafarisayo walikuwa wanasikiliza (Fungu 14).

Uadilifu anaoungelea Yesu katika mfano huu, ni kuwa huwezi kumtumikia Mungu na pesa kwa wakati mmoja; utajikuta umejitoa zaidi kwa mojawapo, ama Mungu au fedha (fungu 13). Kama unapenda fedha huwezi kumpenda Mungu. Mafarisayo waliyasikia yote lakini hawakujizunza chochote. Badala ya kutumbu ili bimgu zifurahie, wao walimdhihaki Yesu. Maneno yake yalikuwa ujinga mtupu kwao, kwa kuwa walipenda fedha (fungu 14). Kwa kujibu dhika zao Yesu aliwaambia “Akawaambia, Ninyi ndinyi mnaojidai hali mbele ya wanadamu, lakini Mungu awajua mioyo yenu; kwa kuwa lililotukuka kwa wanadamu huwa chukizo mbele za Mungu”. (Fungu 15).

Anaendelea kuwafafanulia kuwa torati na manabii ni mashahidi kuwa ufalme wa mbinguni umefika na kila mtu anajaribu kujipenyeza kwa haraka kwenye ufalme (Fungu 16-17). Kwa muhtasari anasema “Kwa kuwa mnatukuza mambo ya wanadamu badala ya mambo ya Mungu, hivyo mnaukataa wito wa Mungu wa kuingia kwenye ufalme, na wito huo unafanyika kupitia kwangu”.

Ujumbe unaofuata (fungu 18), ambao unaeleza taraka na uzinifu unaweza kuonekana uko nje kabisa na mada iliyokuwa ikijadiliwa. Lakini ni endelezo la ufafanuzi kuwa torati na nabii ni sehemu mojawapo ufalme wa Mungu, na katika kumkataa Yesu mafarisayo wanaterekeza torati na nabii, ambazo zinawaelekeza kwake na katika kutenda hayo, wamemkataa Mungu (ni hili linafananishwa na uzinifu katika vitabu vyote vya agano la kale; angalia Yeremia 3:6 n.k.). na sasa kama kielelezo cha neema ndio anawapa mfano wa Lazaro na tajiri.

Kisa cha kutoamini:

Katika mfano hii wapo wahusika watatu, Tajiri (anayewakilisha mafarisayo wanaopenda fedha), Lazaro ambaye ni ombaomba (anayewakilisha kundi la watu wanaodharauliwa na mafarisayo), na Abrahamu (ambaye kifua chake au mapaja yake yalichukulia na wayahudi kama chanzo cha faraja katika maisha yanayokuja).

Na katika mfano huu Yesu anaendelea kusisitiza mada moja tu. Kwamba mnapenda kujikweza na kujiweka kama watu wajuu waliobarikiwa na Mungu, lakini hali harisi ni kuwa mnapenda fedha na mnamchukia Mungu – na ndio maana ninatumia muda wangu mwingi kushiriki neno la Mungu na watu mnaowaona waovu, ndio maana mnawatenda wanadamu wenzio, na hmnyenyekei na kuamini kuwa mimi ili mpate utajiri wa kweli.

Turejelee mfano huu. Ombaomba anafariki. Na yesu bila kusita anawaudhi mafarisayo kwa kueleza "…..akachukuliwa na malaika mpaka kifuani mwa Ibrahimu." (Fungu 22). Hii kama ilivyo kawaida na mifano ya Kriseto ni kinyume na mategemeo la mafarisayo walilotegemea lingetokea kwa mtu kama Lazaro. Watu kama hawa walikuwa maskini na ombaomba kwa kuwa walikuwa chini ya laana ya Mungu, huu ndio ulikuwa msimamo wa mafarisayo, kwa hivyo ilikuwa wazi kwamba watakapofariki watupwe jehanamu waendelee kuhangaishwa na moto wa milele. "Lakini sio hivyo" Yesu asema maoni yenu ni kinyume na mafunzo ya kweli. Hamjui lolote kuhusu ufalme wa Mungu. "Sio kwamba tu mmekosea katika maoni yenu kuhusu hisia za Mungu kuhusu ombaomba huyu bali mmekosea kuhusu hisia za Mungu kuwahusu pia".

Yesu anamalizia mfano wake wa kinyume cha mategemeo yao kwa kuwaambia kuwa hatimaye tajiri akafariki, na akazikwa , lakini yeye tofauti na ombaomba kama walivyokuwa wanategemea ndiye aliyetupwa jehanamu na kutesekea huko. Na kwa maelezo ya Yesu, kutokana na mateso anayopata, akaangaza na kwa mbali akamuona Ibrahimu wakiwa na Lazaro pembeni mwake. Tajiri akalia "baba Ibrahimu, ni hurumie, mtume Lazaro andumbukize kidole chake kwenye maji baridi, aje aupoze ulimi wangu; kwa kuwa ninaumia na miale hii ya moto" (Fungu 23-24). Lakini Ibrahimu akamjibu "….. Mwanangu, kumbuka ya kwamba wewe uliyapokea mambo mema yako katika maisha yako, na Lazaro vivyo alipata mabaya; na sasa yeye yupo hapa anafarijiwa, na wewe unaumizwa" . (Fungu 25).

Baadae anatoa maelezo ya ziada "Na zaidi ya hayo, kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze; wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu". (Luka 16:26). Labda inaeleweka kwa nini mtu angependa kuvuka kutoka "kule kuja huku" lakini ni vigumu kuelewa kwanini mtu avuke kutoka "huku kwenda kule", Ibrahimu anamweleza Lazaro kwanza kwa kumuita "mwana" halafu kumueleza ilivyo ngumu kutoka upende mmoja kwenda mwingine kwa sababu ya ufa uliopo.

Daraja la kuvukia ufa:

Yupo mmoja tu aliyekivuko cha wenye dhambi. “”Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yupo mmoja tu aliyekivuko cha wenye dhambi. “”Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana Mtakatifu 3:16). Mungu alimtoa Mwanae kama patanisho sio kwa wenye dhambi tu kama Lazaro hata kwa wenye dhambi kama Yule tajiri pia. Lakini tajiri hakumkiri wala kumpenda Yesu. Tajiri alipenda tu aliyokuwa anayapenda raha, starehe kwa kuwanyanyasa wengine ambacho ni kinyume na mapenzi ya mwana wa Mungu.

Yesu anakamilisha hukumu yake dhidi kutokuamini kwa mafarisayo kwa tajiri kuomba mtu atumwe kwa nduguze, ili wasije wakajikuta katika mahali alipo yeye. “Ibrahimu akasema, Wanao Musa na manabii; na wawasikilize wao”. (Kumbuka maneno ya Yesu katika fungu la 16-17? Kwamba torati na manabii wote wanamshuhudia yeye. Angalia Johana 5:45-47 na Luka 24:44-47).

“Akasema, La baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokae kwa wafu, watatubu” (Luka 16:30) “Akamwambia wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishiwa hata mtu akifufuka katika wafu” (Luka 16:31). Na ni kweli hawakusawishika, mafarisayo waliungana na waandishi na kuhani wakuu wakamsurubisha Yesu, wakajaribu kuwasawishi askari wadanganye kuhusu kufufuka kwake (Mathayo 27:62-66) na zaidi ya hayo wakaendelea kuwatesa waliomkumbali na kumwamini Yesu.

Kipo kivuko kinachowasaidia wenye dhambi kuvuka ufa uliopo. Kuvuko hicho ni Yesu Kristo. Lakini tajiri (wayahudi walipinga Yesu Kristo na kukataa kumtambua kama kivuko) hakutaka kuweka imani yake ndani ya Yesu. Ningeruhusiwa ningeweka maneno ya Ibrahimu kama ifuatavyo:

“Angalia rafiki yangu, ulikataa kuja kwake Yesu, na kwa kukataa kwako, hakuna nafasi iliyobaki bali na ulipo. Hata sasa hujakumbali kwamba unahitaji msamaha. Bado unayapenda uliyoyapenda mbeleni – kila mtu akuhudumie, akutegemee. Huwezi kuvuka kuja huku kwa kuwa huwezi kujishusha, ukanyenyekea kama alivyokuwa anayenyekea lazaro uliyemjua. Wewe kwa matendo yako ndiye uliyetengeneza ufa unaouona katika yako na Kristo kwa kuwa hukumwendea upate maisha.

“Bado unafikilia kama ulivyokuwa unafikilia tangu mwanzo – kwamba wewe ni wa maana na Lazaro hana dhamani yoyote, alikuwa kama uchafu chini ya miguu yako. Na sasa ndio umeona ila hujaelewa kuwa muda wote ule ule umekuwa sio mtu wa muhimu kama alivyokuwa Lazaro, na kwangu mimi anayedhaminiwa ni yule ambaye hadhaminiki, na wewe sasa uko vile umekuwa maisha yako yote kwamba si chochote, si chochote kinachodhaminika.

“Sasa ni nii hii” ambacho unataka lazaro aende akaonye ndugu zakowalio kama wewe? We unacheza nini? Hawatasikiliza. Wako na Musa na nabii ambao wameshawatangazia ujio wa yesu. Kama hawatawasikiliza wao, kinachokufanya ufikirie watamsikiliza Lazaro ni nini? Sahau kabisa, je kinachokufanya ufikilie kuwa mtu akifufuka watamsikiliza ni nini? Ni vema utambue unacho kiomba kilifanyika kwa Yesu, alifufuka na hata baada ya kushuhudia yote hukuamini na ndio maana uko hapo ulipo kwa kushidwa kuweka imani yako kwake.”

Hata kama hukufurahishwa na ufafanuzi wangu wa mafungu haya, tunakumbaliana kitu kimoja cha msingi, sio mwenendo mzuri kuchukulia fungu moja na kujaribu kujenga hoja kwa kulitumia fungu hilo moja tu, hasa pale fungu hilo linatumika kutoa mfano kueleza jambo linguine tofauti kabisa. Mfano huu kinsingi unatolewa kuhusu viongozi wa kiyahudi waliokataa kumwamini Yesu na wengine wasio onekana kustahili waliomwamini na kumkiri Yesu. La pili kuonyesha kuwa utajiri sio lazima ni Baraka inayotokana na Mungu kama walivyoamini wale wayahudi.

Mfano huu haujawekwa hapo kutuonyesha hali ilivyo mbinguni na jehanamu. Ni mfano wa kutuonyesha hukumu dhidi ya viongozi wa wayahudi wasioamini, matajiri wasiojali, kwa kutumia mifano walioielewa wayahudi ya (“Jehanamu na kuwa na Baba Ibrwahimu”) ili kutoa msisitizo, kwa njia nyingine, Yesu hakuwa anahalalisha imani yao kuhusu maisha ya baadaye, bali alikuwa tu akitumia mfano ambayo ungeelewaka kwao kirahisi.

Haukuwa wajibu wake yesu kutueleza mambo tunayotamani kuelewa ya itakavyokuwa mbingu na jehanamu, bali wajibu wake ulikuwa kutufunulia siri za Mungu (Warumi 16:25, Waefeso 1:9 n.k.), fumbo la miaka yote (Waefeso 3:4-5) kwamba ndani yake, Kristo, Mungu amekuwa akiurejesha ulimwengu kwake (2Wakorintho 5:19). Mawazo yetu ya kiulimwengu huwa yanatupeleka nje ya suala la msingi ambalo pia tajiri katika mfano huu alilikosa: Amini aliyefufuka kutoka kwenye wafu.

Nani amepotea?

Hakuna aliyepotea tofauti na wale wasiomwamini Kristo. Kwa kuwa Mungu aliuumba alimwengu na akasema unapendeza (Mwanzo 1), na akasema viumbe “vinapendeza sana” (Fungu 31), na kwa kuwa Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtuma mwanae ili atakaye mwamini apate uzima ule wa milele (Yohana 3:16), si fikra potovu kufikiria ya kuwa Mungu atatengeneza fursa kwa kila mwanadamu to sikia na kuamua kufuata injili, na kwa kuwa wengi hufa kabla ya kuisikia injili, sio wazo potovu kufikiria kuwa Mungu atawapa fursa hata baada yao kuwa wamefariki.

“Sio kwamba ni wazo potovu, lakini hii sio kusema ni kweli”

Ndio unaweza kuwa sahihi katika hilo. Lakini neno la Mungu, tunakumbaliana ndilo sahihi. Na neno la Mungu ni habari njema kwa wanadamu, sio habari mbaya kwa wanadamu. Na kilichochema kwa wanadamu ndio mapenzi ya Mungu kwao. Na Mungu amedhihirisha

mapenzi yake kwa wanadamu kwa kumtuma mwanae Yesu Kristo. Mapenzi yake sio ulimwengu uangamie bali uokolewe (Yohana 3:17).

"Nina kiri sio haki kwamba watu ambao hawakupata fursa ya kuisikia injili kabla ya kufa kwao wapotee, lakini kama jambo sio haki kwetu sio kusema sio haki machoni mwa Mungu. Kama Mungu angependa kuokoa wachache tu, hiyo iko ndani ya uhuru wake. Zaidi ya yote, wanaohukumiwa wanapata kilicho cha haki kwao."

Hatujengi hoja juu ya hili. Hakika Mungu angependa, angefanya mambo hivyo. Hoja tunayojenga ni kwamba Biblia haimuonyeshi Mungu kama wa namna hiyo. Inamuonyesha Mungu kupitia kwa Kristo kama 1: Aliyejaa neema na anayeendelea kwa uaminifu kutafuta upatanisho na kila mwanadamu (1 Yohana 2:2).na 2: kwa neema anayetamani wokovu wa kila mwanadamu (1 Timotheo 2:3-4).

Kina cha desturi ya maandiko

Kina na desturi ya maandiko sio kitu kingine bali injili. Maandiko yapo, au tunaweza kusema ni ushuhuda wa wa injili. Biblia, kwa maneno mengine, ni ufunuo kupitia kwa Roho Mtakatifu wa neno la Mungu kuhusu urejesho na ukombozi kwa neema kupitia kwa imani kwa mwanae Yesu Kristo aliyefanywa kama mwanadamu kwa ajili yetu.

Biblia, ambayo ni ushuhuda wa habari njema kwa wanadamu, inamdhihirisha Mungu kama alivyo, Mungu muumba, anarejesha na kuokoa. Biblia iliyofunuliwa kwa Roho Mtakatifu, inatueleza kuwa Mungu anapenda alivyoumba, viumbe ambavyo yeye ni mkuu, na mwenye uwezo wote, na pia anapenda watu aliowaumba. Aliumba vyote, hata wanadamu, akaona vinapendeza (Mwanza 1:31), na kwa kuwa wanadamu walivuruga, Mungu kupitia kwa Yesu Kristo kutoka mwanzao wa ulimwengu (1Petro 1:20), aliupatanisha ulimwengu naye (Warumi 5:10).

Biblia inatwambia Mungu anatamani wanadamu watumbu na wamrejelee (Matendo ya Mitume17:20; 2 Petro 3:9). Wanatamani wamjue na wawe na uhusiano kwa kumjua alivyo kama muumba wao, mkombozi, anaye rejesha, baba na rafiki. Anapenda waishi milele ndani yake na wawe naye.

Mtume Petro aliandika: "Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba". (2 Petro 3:9). Hivi ndivyo Roho Mtakatifu unamdhihilisha Mungu mara kwa mara anavyo hisi na kufikiria kuhusu watu anaowapenda. Aliwaumba kwa mfano wake; akageuka wakawa wadhambi, wakajitenga naye, na yeye kwa kuwapenda kwa kina hata wakati wakiwa waovu (Warumi 5:6-8), amewasamehe na kuwarejesha kupitia kwa damu ya mwanae (Yohana 12:32; I Yohana 2:2).

Hakimu ni Mwokozi

“Ulisema kuwa lipo fungu linguine linalotumika mara kwa mara kuonyesha kuwa wanaokufa bila kuijua injili huwa wamepotea”

Nashukuru kunikumbusha. Fungu la pili ni hili: “”Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu; kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu.” (Waebrania 9:27-28). Njia tu ya kuelewa fungu hili kuwa linamaanisha waliokufa bila kuisikia injili ni kulisoma huku unawaza hivyo.

Kwa njia nyingine, fungu lenyewe hata halisemi hivyo, na hata halijibu swali hili la kufa bila kuisikia injili. Kwa kifupi linasema hukumu inafuata kifo. Halisemi hukumu hiyo inazingatia nini, wala kama Mungu atawaruhusu wanadamu kumwamini baada ya wao kufa. Fungu halifafanunui kwa vyovyote vile kama wanadamu wanayo nafasi ya injili baada ya kufa.

Basi tuendelee. Tunaambiwa katika matendo ya Mitume 17:30-31: “Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu Yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu.”

Si tu kwamba ulimwengu utahukumiwa katika utukufu, bali utakuhumiwa sin a mwingine ila mwokozi wa ulimwengu, Yesu Kristo. Mungu haamrisha tu kila binadamu kutubu, anafanya hivyo kwa kuwa amemteua Yesu, aliyekufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote awe hakimu (1 Yohana 2:2).

Na kama kuna yeyote anayetafuta dhibitisho kuwa Mungu ana nia ya dhati ya msamaha na urejesho wa wanadamu wote, analotakiwa kutambua ni kuwa alimfufua kutoka kwa wafu hata baada ya waliokuwa wafaidi wokovu (yaani sisi wote) kumuua. Malengo ya Mungu kwa mapatano ya kuwa Mungu wetu na sisi watu wake hayawezi kukatizwa.

Ufunuo 20 inaielezea hukumu ifuatavyo: “Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheup, na yeye aketiye juu yake, ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi, na vitabu vikafunguliwa;

Na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika vile vitabu, sawasawa namatendo yao. Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na Mauti na kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. Mauti na kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.” (Ufunuo 20:11-15).

Baada ya hukumu, kila mmoja anaokolewa au anahukumiwa. Lakini kwanza kabla ya utenganisho wowote kufanyika, la kushangaza kila mwanadamu, kifo na jehanamu vyote viwili vinatupwa kwenye moto. Labda kama ningeruhusiwa kwa muda tu kuvipatia kifo na jehanamu kiwiliwili, hebu fikiria vimekaa katika mahakama, bila uwezo wa kuficha hisia zao, na vikijua fika kila mmoja ametenda dhambi. Wakingojea hukumu, mawazo yao yametekwa na ugumu na mateso yanayowangoja yasiyohesabika.

Gafla, hukumu yao inapitishwa na malaika wenye nguvu za kutisha wanawabeba kutoka mahakamani huku wakilia, wanawatupa kwenye shimo lenye kina kirefu, na moto mkali. Ukimia unatanda mahakamani. Hii inaweza kumaanisha nini? Kama kifo na jehanamu vimeharibiwa, je itakuwaje mtu abakie kuwa mtumwa wao?

Wote wamehukumiwa

Bibilia inafundisha kuwa ipo njia moja tu ya kuokolewa – Kupitia kwa neema ya Mungu ndani ya imani katika Kristo (Matendo ya Mitume 4:12). Kama tunavyoona kutoka Ufunuo wa Yohana na vifungu vingine, kama vile Mathayo 25:31-33, kutakuwepo watu aina mbili katika hukumu ya mwisho, wanaookolewa na wanaohukumiwa. Kwa hali hiyo je, itakuwaje kwa wale ambao hawajawahi kuisikia injili kabla ya kufa kwao? Wengine wanaeleza kuwa hao watu wamehukumiwa milele kwa kuwa hakuna mkristo aliyewahi kuwajulisha kuhusu kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo.

Fikiria ujumbe wa Paulo katika Warumi 10:14-21. Hapa Paulo anaelezea kutoamini kwa wana Israeli akinukuu vitabu vya zaburi na Isaia. Kwanza, anauliza swali kuhusu kusikia kwa neno la Kristo (Fungu 17-18), "…….. Lakini nasema, Je! Wao hawakusikia? Jibu lake "Naam, wamesikia" kwa (Ananukuu Zaburi 10:18) "……Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu." (fungu 18).

Linalofuata, Paulo ananukuu nabii Isaia kuonyesha kejeli ya wanaisraeli kutoamini dhidi ya wokovu wa watu wa mataifa "Na Isaiah anao ujasiri mwingi, asema, Nalidhihirika kwao wasiouniulizia" (Fungu 20, akinukuu Isaia 65:1). Neno la Mungu ni neno la wazi kwa mataifa yote; sio kwa wale tu ambao wamejaliwa kukutana na wamisionari na waijilisti. Yesu ni mwana wa Mungu na pia neno la Mungu – Taarifa kuu kuhusu wema wa Mungu kwa muda wote uliopita na muda ujao na linaloenea katika kila kona ya ulimwengu huu.

Inashangaza kuwa tunasisitizwa tuamini kuwa Mungu hana uwezo wa kueneza injili kwa njia ambazo hatuelewi na kwa njia ambazo sio lazima tuhusike. Katika maelezo kwenye maandiko, Roho Mtakatifu anawakilisha upatanisho wa Yesu kama ambao unatosha urejesho wa kila mwanadamu katika ulimwengu wote, ulimwengu ambao Kristo ameushikilia katika kiganja cha mkono wake kwa niaba ya baba yake ambao anatoa uhai na uwepo kila wakati. Na zaidi ya hayo, tunaombwa tuamini, kama mhubiri mmoja alivyosema, kuwa "Mamilioni wanaelekea jehanamu wiki hii kwa kuwa hakuna mwijilisti anayewafikishia injili!"

Mungu hajichanganyi katika neno lake – hataki mtu yeyote apotee. Yesu alisema atawakusanya wanadamu wote kwake. Kwa kuwa wokovu huwafikia sio kwa njia nyingine bali kuamini neema ya Mungu kupitia kwa Yesu Kristo, hii ina maanisha Mungu hufanya kwa muda na kwa njia tusizozijua, anapatia kila mwanadamu nafasi ya kukumbali neema ya Mungu kupitia kwa imani katika Kristo.

Hakimu mtakatifu

Tukirejelea Ufunuo 20:11-15, tunaona ukweli uliowazi kuhusu hatima ya wanadamu, ambao unaelezwa mara kwa mara katika maadiko, kwa wakati mwingine ikituhimiza 1) Wote, yaani wanadamu wote wanahukumiwa, hakuna kubagua 2) Yesu ndiye hakimu.

Kwa utulifu ngoja sasa tujaribu kuyatilia maanani haya maneno. Yesu ni hakimu wa aina gani? Kwa hakika yeye sio kama hakimu yeyote wa kibinadamu ambaye tulishawahi kukutana naye, au tutakuja kukutana naye. Hakuna hakimu wa kibinadamu ambaye anaweza kuchukua nafasi ya mtuhumiwa na halafu baadaye kumtangaza "mwenye haki au asiye na kosa!" Lakini Yesu alifanya hilo. Kwa kweli ameshalifanya. Na alilifanya tangu misingi ya ulimwengu kuwekwa. Hii ina maana mpango wa ukombozi uliwekwa hata kabla ya Adamu na Eva kutamani lile tunda katika shamba la edeni.

Huyu sio hakimu wa kawaida. Huyu hakimu anashikilia ulimwengu ka njia ya muujiza na ulimwengu uliumbwa kwa neno la mdomo wake. Hakimu huyu hakuhakikisha tu uwepo wetu bali alishuka akawa mmoja wetu, kwa nia ya kutoa msamaha wa dhambi zetu dhidi yake na pia kutupatia maisha ya milele ndani yake. Huyu hakimu anavuta wanadamu wote kwake, waume, wake na watoto kupitia kwa kifo chake na kufufuka kutoka wafu. Huyu sio hakimu wa kawaida.

Yeye amekamilika kwa uadilifu na haki, lakini sio tu kuwa mwadilifu na mwenye haki tu, kwa kuwa kutenda haki kutuacha wote tumekufa, bali uadilifu wake na haki yake zinazidiwa na huruma zake (Hosea 6:6; Mathayo 9:13; 12:7; Yakobo 2:13). Amepitiliza kipimo, kupitia kuuchukua mwili wa kibinadamu, ili kuhakikisha wanadamu wanaokolewa. Alichukua dhambi zetu zote na kuharibu dhambi katika mwili (Warumi 8:3). Huyu sio hakimu wa kawaida.

Huu ulimwengu unachimbuka kutokana na neema ya uhuru wa nafsi tatu za Uungu. Kupitia kwa neema yake ulimwengu unakuwa. Kupitia kwa neema yake mwana akawa na mwili kama wa mwanadamu kwa ajili yetu, akawa patanisho la dhambi za ulimwengu mzima, ili kusudi la Mungu kwetu litimilike ndani yake, mwana aishiye milele, Yesu Kristo.

Wanadamu wote watakapo kusanyika kutoka ulimwengu mzima, wakubwa kwa wadogo (Ufunuo 20:12), pamoja na waliokufa (fungu 12-13), watakaposimama mbele ya kiti cha hukumu, watakuwa wanamtazama sio mwingine bali Yesu Kristo. Hebu tafakari sehemu hiyo ya tukio. Hakimu wao, ambaye ndiye anashikilia maamuzi ya maisha yao milele mkononi mwake, sio mwingine bali ni kondoo wa Mungu, sadaka ya upatanisho sio tu kwa ajili ya dhambi zetu bali pia kwa dhambi za ulimwengu mzima (1 Yohana 2:1-2). Wako mikononi, mikono

iliyodungwa, ya mwana wa Mungu aliyefufuka, aliyesurubishwa na aliyetukuka – Kristo. Wako katika huruma zake- katika huruma za anayebuni huruma.

Siku ya hukumu

Fikiria kwa muda kwamba umeketi kwenye mahakama ya mbinguni, ukimsubiri hakimu, mapigo ya moyo yanaongezeka kwa kujua unamsubiri hakimu wa yote aingie ili akuhukumu. Hujawahi kufikiria kwa kina kuhusu hukumu ya mwisho. Huwa unasikia watu wanaongea kuhusu Mungu na mambo kama hayo, lakini haina maana kubwa sana kwako.

Sasa unagundua wakati umefika uwajibike kwa matendo yako. Siku ya malipo imetimia, hatimaye. Huna amani. Pumzi linakupungukia, mapigo ya moyo nayo yanaongezeka, jasho linakutoka. Macho yako yanaangaza ile milango miwili iliyonyuma ya kiti cha hakimu. Juu ya mlango mmoja pameandikwa "Sehemu ya kutokea kwa watakatifu walio safi". Ya pili imeandikwa "Sehemu ya kutokea kwa wengine wote". Akili yako inarejelea maovu yote katika maisha yako; uongo, kutamani mambaya, kujipenda, kusariti, urafi, uroho, ubinafsi n.k. Na sasa ndiyo hii siku imefika. Unajisikia umechoka akili. Huna tumaini lolote. Ndani yako unajiskia uchungu.

Hatimaye hakimu anaingia na kuchukua nafasi yake. Uwepo wake unakuwa mzigo kwako. Alivyo ni tofauti na ulivyowahi kufikiria. Ukumbi wa mahakama unamkaribisha na kupendezwa naye. Ni kielelezo cha nguvu na uwezo, na mng'ao wake unaonyesha amani, utulivu na upendo. Mawazo yako yanahama, sisi huwazi tena kuhusu tishio la kuhukumiwa. Unapata utulivu usio wa kawaida, hisia za furaha zinaibuka kutoka ndani yako. Pamoja na hisia za heshima iliyochanganyika na hofu, unashawishika kumkumbatia badala ya kuishi tena bila yeye. Umepata hakikisho la pekee ndani mwako kuwa hukumu atakayopitisha dhidi yako itakuwa nzuri, na kumtazama tu huogopi chochote.

"Je! Unayakubali mashtaka kama yalivyo?" Hakimu anakuuliza. Sauti yake unakufanya utikike na midomo yako inalazimika kusema ukweli "Nakubali hatia" unajibu, na unapojibu unagundua mambo mawili kwa pamoja, kwanza unaona aibu kwa maisha yako uliyoishi na pili hakimu amekuondolea mashtaka yote. Aibu yako inageuka na kuwa machozi ya furaha na shukrani, unapata amani moyoni unapoona anavyo kuangalia kwa upendo wa pekee.

"Makosa gani unakiri?" Hakimu anakuuliza, na tabasamu ya utani, "Sioni kumbukumbu ya kosa lolote katika nyaraka zako za mashtaka." "Je! Uko tayari kuungana na wengine kwenye sherehe?" "Sawa twende kwenye sherehe!" anafungua mlango ulioandikwa "Sehemu ya kutokea kwa watakatifu walio safi" na anakupa ishara kuwa upitie ule mlango pamoja naye.

Au, ungeweza kukataa mashtaka na kujaribu kujitetea, ombe kupewa nafasi ueleze ulivyosafi katika maisha yako. Ujaribu kueleza michango uliotoa kwa matumizi ya kazi ya bwana na pia kwa wasiojiweza, au bado pia uombe uachiwe huru kwa kuwa hata Mungu hana haki ya kukuwekea shereia za kukubana.

Au bado pia, unaweza kumuomba akuache, injili yake haihitaji, mapendekezo yake kuhusu unavyotakiwa kuishi hayakuhusu, ungependa ufanya yale yanayokusaidia kuishi katika ulimwengu huu wa dhuruma, kwa kuwa umejifunza kuishi na kuweza kujinasua katika nyakati ngumu. Haya yote yanakusaidia kujiona kama mshindi, na kuchagua pakuishi hata kama gizani, ukiwa huru bila kuhurumiwa na yeyote.

Hakuna hata ya kuhofia

Hata kama hujafurahishwa na mfano wangu wa mahakama ya mbinguni nilioutoa hapo awali, cha msingi ni kuwa hakuna sababu ya kuhofia kwamba wapendwa wetu waliotangulia, au hata mtu yeyote aliyefariki wameelekezwa kwenye moto wa milele kwa kuwa hawakufikia na wamisionari na ujumbe wa injili kabla ya kukutana na mauti. Yesu anaijua injili pia, na kwa uhakika zaidi ndugu na dada, anaweza kuineza injili vizuri zaidi kuliko vile sisi tunaieneza.

Nasitikika kusema lakini, Biblia unatwambia kuwa wengine hawataikumbali neema tunayopewa na muumba na mfalme wetu (Mathayo 25:46; Ufunuo 19:20; 20:15). Hawatamwamini mwana wa Mungu na pia Mungu mwenyewe. Na hakuna hatari inayoizidi hiyo, hakika hakuna ujinga zaidi ya kukataa mwaliko wa kuingia kwenye sherehe ya harusi ya mwana kondoo ambayo ni haina malipo ili kujaribu kufanya maisha ambayo tayari hayana maana kuwa na maana. Na hicho ndicho ubinadamu wetu unajaribu kila siku kufanya.

Akili yetu yenye upeo mdogo inaona ni vigumu kubeba mayai yetu kwenye kapu moja, inatuonyesha ni hatari kuamini kuwa neema itatufikisha, je nayo matendo mema tuliyoyafanya hayatatambuliwa? Kwamba tunashidwa kuamini kuwa sio kwa lolote bali ni kuamini neema ya Mungu kupitia kwa mwanae yesu Kristo.

Lazima pawepo na njia ya kuonyesha tofauti katika ya wale wanaostahili, “kama sisi” na kutofautishwa na “wale” wasiostahili kama wale “wavuta bangi”, waliokaa kwenye kona. Lazima iwepo njia itakayowapa watu wema, watu wazuri nafasi nzuri kuliko hawa waovu. Hii neema ya bure inaacha maswali mengi mno bila majibu na inakuwa ngumu kwetu sisi kuiamini. Hii ni neema ya Mungu ambayo haifuati mfumo wa uelewa wa wanadamu, uelewa wake uko juu kama ilivyo mbingu juu ya ardhi. (Angalia Isaia 55:8-9 na Zaburi 103:11-14).

Vitabu viwili tofauti

Kitu cha ajabu kinatokea katika mtililiko wa hukumu hii ya mbinguni katika kitabu cha Ufunuo 20. Kwanza, wafu wanakusanywa na vitabu Fulani vinafunuliwa (Ufunuo 20:12). Halafu kitabu kingine kinafunuliwa, mara hii sio vitabu bali kitabu, hiki kitabu cha pili ni tofauti na vitabu vilivyofunuliwa mwanzoni. Hiki kitabu kinaitwa kitabu cha uzima. Halafu hawa mafu wanahukumiwa “kulingana na matendo yao, kutokana na mambo yaliyoandikwa kwenye vitabu.”

Hivi “Vitabu” ndivyo vyenye kumbukumbu ya matendo yao, ushahidi wote unaohitajika kuwahukumu, na kutokana na ushahidi huu, we unafikiri utawaacha wapi? Kwa kawaida

ushahidi uliopo utawaacha mahali wewe na mimi tulipo “wenye hatia”. Hii ndiyo hali mbaya ya kila mmoja wa hawa wafu, na kwa kweli ndio hali ya kila mmoja wetu ambaye aliwahi kuishi katika ulimwengu huu.

“Hakuna aliye mtakatifu, hakuna hata mmoja” asema Bwana. “utakatifu wenu ni kama matabara machafu” Je, hii ndiyo hali halisi ya tulipo katika hukumu? “wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Bwana”, kama yupo anayejiuliza “nani aliyefanikiwa” na ni nani hakufanikiwa.

Kwa hakika ni vema tuelewe kuwa hakuna hata mmoja ambaye yuko nje yah ii hukumu, na zaidi tunaambiwa kila mmoja ambaye tayari amekufa yupo: bahari inatoa wafu wote ndani yake, kifo na jehanamu navyo vinatoa wafu waliomo (Fungu 13). Usipate wazo kuwa yupo hata mmoja ambaye amejificha. Kila mmoja anasimama mbele ya kiti cha hukumu. Na wote wanahukumiwa “Kulingana na matendo yao”.

Kwa wakati huu, unaonekana mwelekeo sio mzuri. Hakika hakuna aliyemtakatifu. Kila mmoja ambaye aliwahi kuishi na kufa, ameshutumiwa na matendo yao kama ilivyonukuliwa kwenye vitabu. Na kila mmoja amesimama hapo akingojea hatima yake wakati huo kifo na jehanamu vinaharibiwa. (Fungu 14).

Lakini ngoja! Ni nini hii? Kile kitabu “kingine” kinakuja tena. Hukumu kulingana na matendo yao kama ilivyonukuliwa katika vitabu sio mwisho!, kipo kitabu kingine, kitabu cha uzima, na wale wote wanaoishia motoni pamoja na kifo na jehanamu ni wale ambao majina yao hayapo katika katika kitabu hiki (Fungu 15)! Muda wote huu kitabu hiki kimekaa tu! Kila mtu ambaye jina lake lipo kwenye kitabu hiki anapata msamaha. Na je, majina yanaingizwaje kwenye kitabu hiki? Kwa kupitia damu ya upatanisho ya Kristo. Fumbo kuu ni kuwa kupitia kwa upatanisho wa Kristo, jina la kila mtu lipo kwenye kitabu cha uzima. Waumini huwa tu wanapokea kilichokuwepo tangu mwanza.

“Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali maepita kutoka mautini kuingia uzimani.” (Yohana 5:24. Wale ambao hawataamini, kwa hali nyingine hawataweza kuvuka. Hii ndio ujumbe wa maandiko tangu mwanzo, katika agano la kale na hata agano mpya- ndio ujumbe wa Yesu Kristo. “Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima.” (Yohana 5:39-40).

Ipo njia moja tu ya kuokolewa – Imani katika Kristo. Sheria ile ile inayotuhukumu kwa kushindwa kutii, hiyo hiyo inatuletea wokovu kwa kutangaza kuwa Mungu atatuma mwanae kutukomboa kutokana na dhambi. Laana ya kifo sio neno la mwisho. Ndani ya Kristo, kila kitu kinafanya upya. Neno la uhai lililo ndani yake ndilo neno la mwisho katika maisha ya binadamu!

Karibisho la Wenye dhambi

Katika kitabu cha Mathayo 25:31-46, kila mtu anakuja mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo. Yesu natumia kigezo gani kutenganisha mbuzi na kondoo? Biblia inatoa kigezo kimoja tu cha wokovu – ni ama ukumbali zawadi ya wokovu ya Mungu au uikatae. Mojawapo ya kitu cha kushangaza katika fungu hili ni kuwa watu walijitoa na kuonyesha upendo wao kwa Kristo walikuwa hawatambui kuwa wanauonyesha upendo huo. Hawakuwahi kujiona kama wao ni wazuri, au wema au hata watakatifu . “Ni lini tulifanya haya yote?” kwa mshangao wanauliza.

Suala la kejeli, wale wanaokataliwa pia wanashangaa, wanashangaa kuwa hakimu hatambui matendo yao kama ya maana kwa Mungu. “Ni lini tulishidwa kukutendea haya yote?” wanauliza kwa mshangao. Wao hawaoni sababu ya kuwa sehemu ya neema ambayo kwao ni ya wenye dhambi. Wao wamekuja na ripoti ya matendo, msururu wa mambo ambayo wanaamini waliyatenda, lakini kinachowashangaza hayonekani kumridhisha hakimu, kwa hiyo wasingependa kuwa sehemu ya ufalme wa watu wasio na matendo mema.

Yote ni Kwa Neema

Ni nani atakayempenda Yesu zaidi – aliyesamehewa zaidi au aliyesamehewa kidogo? Yesu aliuliza swali hilo katika Luka 7:41-50. Suala ni nini? Watu wanaojiona ni wema, ni wanyoofu huwa hawatafuti neema. Watu wanaotambua kuwa wao ni wenye dhambi huwa wanahangaikia neema. Wengi wa wenye dhambi wakubwa wataingia katika ufalme kabla ya wale watakatifu, Yesu akasema (Mathayo 21:31). Aliitwa rafiki wa wenye dhambi na hivyo ndivyo alivyo (Luka 7:34). Yeye ni rafiki na ni wangu, kwa kweli.

Watu wenye dini huwa wanafikiria kuwa wamepewa nafasi ya pekee katika safari hii, wao wanajua ni nani anastahili na ni nani hastahili. Wanatunza mipangilio, ni wazuri, ni watakatifu wao tayari wako ndani, lakini wanaosababisha furugu, wasiotii, wasioolewa, wanaohudhulia sinema, wote hao kulingana na wao wako nje.

“Usijihesabie” Yesu asema “Je! Unafikiri unajua utakatifu? Kwa nini usiniamini niwe utukufu wako, hata kama utukufu wako hautoshi, umeoza na hata husikii. Nitahurumia yeyote nitakaye kwa sababu hiyo wewe uliyekuja kudai kwa sababu ya matendo, chukua matendo yako uliondokee (nisamehe kwa ufafanuzi huo) (Mathayo 20:13-15).

Ni wenye dhambi wangapi waliokufa wakitamani haki, utakatifu, amani, tumaini, ukweli, uhuru, lakini hawakujua vinapatikana wapi? Katika Kristo na katika kristo pekee haya mambo yanatimizwa “Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na yesu Kristo uliyemtuma” (Yohana 17:3).

Kumbuka lililotokea Yesu alipomgusa mwenye ukoma? Kila mtu alikaa mbali na wenye ukoma. Lakini sio Yesu. Hakuogopa kuwagusa na hata alipowagusa, walipokea uponyaji. Mili yetu na mawazo yetu ni kama wale wakoma, bila matumaini, imebondeka, imeoza, lakini yesu

alipojitwika mwili wa kibinadamu, sio tu kwamba akili yake haikuadhirika kama yetu, hata alitumia uwezo wake kuponya yetu.

Uponyaji huo uko wazi kwa kila mmoja wetu. Kinachotakiwa tu ili kupokea uponyaji huo, na kuanza kupata raha ya uponyaji huo na kuingia katika ufalme wa Mungu ni kukubali zawadi ya bure – kuamini katika kifo na ufufuo wa Yesu Kristo kupitia kwa upendo usio kifani wa Mungu kwamba yote yametendeka ambayo yalistahili kutendwa ili tupate nafasi katika ufalme.

Mapenzi ya Baba

Katika kitabu chake cha mwisho mwandishi Narnia kwenye msiruru ya vitabu, "The Last Battle, mwandishi wa kikristo C.S. Lewis anaandika tamthilia inayoigiza hukumu ya mwisho. Lewis ambaye nafahamu fika pendo la mwokozi wetu, anaeleza kuhusu mwanajeshi mmoja aliyefariki akiwa hajamkili Yesu Kristo kama mwokozi wake, ila anaeleza kuhusu neema isiyona kipimo, Wakati Emeth (mwanajeshi katika igizo) alipokutana na uso kwa uso na Aslan (Kristo katika igizo), alitokea kumpenda Aslan, kwa kutambua kuwa Aslan ndilo lilikuwa tumaini lake katika maisha yake yote.

Je! Mfano huu katika igizo inatoa picha ya kweli ya Kristo? Ambaye alitufia wakati bado tukiwa wenye dhambi (Warumi 5:8) anayejua waliowake (2 Timotheo 2:19). Yesu anatuambia kuwa Mungu hakumtuma ili kuuhukumu ulimwengu bali ulimwengu uokolewe kupitia kwake (Yohana 3:17) Yohana anaendelea kutufafanulia kuwa Yesu hakufa kwa ajili ya dhambi zetu tu bali za dunia nzima (1 Yohana 2:2). Je! Yesu huyu ni tofauti na Yesu aliyemtawala wa ulimwengu wa nyakati zote?

Labda mfano wa Lewis katika igizo hauko mbali sana na ukweli. Katika kitabu cha Mathayo 25:31-46, tunajifunza kuwa Yesu anaishi ndani ya walio wake na kazi zake zinatimizwa kupitia kwao hata kama hawaelewi kila kitu kinachoendelea. Je! Tutakuwa tunakosea kufikilia kuwa kupitia kwa neema ya Mungu watu kama hawa wanaweza kuwa wanampenda mwokozi wa neema alifufuka kutoka wafu kama tumaini katika mioyo yao?

Na Je! Tutakuwa pia tunakosea kusema tukisema wale ambao mioyo yao imeegemea mambo yanayompinga Mungu na ufalme wake – yaani kujipenda, kujikweza, wengine wanachuki, wengine wanadharau na kupinga mapenzi ya Mungu na yaliyomema, je tukisema watu wa jinsi hii watakuwa na hofu na kuogopa kukutana naye tutakuwa tunakosea?

Na zaidi ya yote , kuna hili wazo wa kustukiza, ambalo linatokana na mioyo migumu kuyeyeyushwa na neema ya pekee ya Mungu, "Na tazama, wako walio wa mwisho watakaokuwa wa kwanza, na wa kwanza watakaokuwa wa mwisho.". (Luka 13:30)

Mategemeo ya wanadamu kuhusu hati na uhalali wa hukumu yanasukumwa nje na neema ya Mungu. Ushuhuda huu unapatika katika mfano wa watenda kazi walioingia nyakati tofauti tofauti (Mathayo 20:13-15). Huyu ni waajabu kwa kuwa yeye anasamehe pale sisi hatuwezi na

anabariki hata pale hatuoni sababu ya kubariki, anaokoa wasiostahili, na wanaostahili wanaudhika na msamaha anaoutoa na anawaambia wakae kando.

Je! mapenzi ya Mungu ni nini? Yesu akasema “Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele, name nitamfufua siku ya mwisho.” (Yohana 6:40). Sasa wengine wanawaza kuwa wengine wengi wasimuone Mwana na wasimwamini na wasiwe na uzima wa milele na kwa hali hiyo hatawafufua katika siku ya mwisho. Lakini wapeleke mawazo yao mambaya sehemu nyingine sio kwenye ufalme. Biblia haifundishi hivyo.

Kusudi Lingine

Yesu Kristo ndiye sadaka ya upatanisho kwa dhambi za ulimwengu mzima (1 Yohana 2:2). Kupitia kwa Yesu Kristo Mungu anafurahia kurejesha vitu vyote kwake iwe hapa duniani au hata mbinguni kwa kufanya amani kupitia kwa danu ya Kristo iliyomwagika msalabani (Wakolosai 1:20). Wengi wa wanadamu walifariki bila hata kusikia injili. Kwa hali hiyo, tunaweza kuwa hatua yao ya imani au hatua yao ya kutokuwa na imani, ndio inayoamua nafasi zao katika ufalme wa wafu.

Wapinzani wa wazo hili wanatumia wazo kuwa kanisa ni kundi ndogoo la kondoo, kwa hivyo mpango wa Mungu ni kuokoa wachache. Kweli kanisa linaweza kuwa kundi ndogo wakati huu, lakini hatuongelei kanisa la wakati huu tu. Tunachokiongelea ni waliofariki kabla ya kuipokea injili. Tunaongelea viumbe vipya wakati ujao.

Upinzani mwingine ni wale wenye wazo kuwa tukihubiri sana mambo ya neema, tutadhoofisha injili na kwa hilo nasema ni upumbafu. Yesu Kristo ambaye ndiye kiongozi wetu alituagiza tuieneze injili , na kwa kweli huu ni mtisha wa kutosha kwa kila mmoja wetu. Pamoja na yote, aliyejaliwa neema ya Mungu na nguvu ya Roho Mtakatifu, hawezi kuificha bali ataieneza kwa wenzake. Itakuwaje kwa mwenye dhambi aliyesamehewa asiweze kuwajulisha wenye dhambi wengine kuhusu upendo, msamaha na pia urejesho wa Mungu kupitia kwa mwanae Yesu Kristo? Roho Mtakatifu anapoishi ndani yetu, tutakuwaje watu wasiojali kuhusu wengine kuishi katika maisha yasio na uponyaji wa dhambi kutoka kwa mwokozi.

Lakini kusema kuwa Mungu anategemea jitihada zetu ni kutoelewa uwezo wa Mungu. Mungu anatupenda sana hata kuturuhusu kushiriki katika neema yake ili kuleta watu katika imani, lakini tunapaswa kukiri uwezo wetu ni mdogo na vile vile hata sisi anaendelea kutuponya kwa hiyo msaada wetu kwake ni mdogo.

Huu ni ukombozi wa ujumla? Hapana. Mungu anawapa wanadamu nafasi ya kumwamini na hata kutomwamini. Mahusiano yanajengwa kwa kuaminiana, na mwishowe watakaoshindwa kumwamini watatengwa. Biblia inaeleza wazi kuwa wanadamu wengine wataamua kutoamini msamaha wa Mungu, lakini kwa hiari yao, pamoja na zawadi ya Mungu ya wokovu watabaki kuwa maadui wa Mungu.

Lakini kwa mawazo hayo, tusije tukajichanganya kuona kama jehanamu ni mahali sawia na mbinguni. Jehenamu ni mahali pandogo tu penye giza ambapo huwezi kupalinganisha na ukubwa wa ulimwengu mzima ulioundwa kwa neema na mng'ao wa Kristo. Wanaochagua kwenda huko hawachagui kwa kuwa Mungu anapenda wawe huko lakini Mungu kwa neema yake ya bure anawaruhusu kuamua kutopokea upendo wake na kwa hali hiyo kuchagua kuelekea mahali walipotengeneza wenyewe kwa kupenda kwao.

Nimepokea barua nyingi zinazopinga wazo hili, pamoja na kupinga nyingi za barua hizi zinakubaliana na maandiko yanayotuelekeza kumwamini Mungu na hasa kuamini hukumu za haki kwa wanaofariki bila kupokea injili ya Yesu. Mimi naona kuwa atawatendea kulingana na uaminifu na huruma zake kama inavyoonekana katika ukuu wa Kristo kama hakimu mkuu.

Sio "Dini"

Jambo la kustaajabisha kuhusu ufalme wa Mungu ni kuwa mfumo wake haufananini na dini, taasisi au kama jamii au hata klabu fulani. Katika dini na taasisi za dunia hii wahusika huwa wanajenda visuizi na sheria ili kuzuia watu kuingia. Lakini mfumo wa ufalme wa Mungu unampangilio wa kuhusisha kila mmoja – kila mmoja aliyeumbwa na Mungu.

Kila mmoja amezaliwa kwa sababu ya Kristo, akiwa na wito wa pekee wa kuingia katika ufalme wake, lakini ni kwamba watu hawajui wito huo kutoka mwanzo. Wengine baada ya kugudua wito huo huwa wanaukataa, wanayo mambo mengine ya muhimu kwao kutekeleza badala ya kufuatilia ufalme. Wengine wanatambua ufalme lakini wanazo njia mbadala za kuingia ufalme huo badala ya mlango pekee uliotengenezwa wa kuingilia, wanaufanyia kazi badala ya kuupokea kama zawadi. Mwishowe, watakaotengwa na kuzuiliwa kuingia ni wale walioukataa kuukumbali kama zawadi ya bure, kwa watu wasiostahili lakini wanaoamini na kutegemea neema ya Mungu.

Sio ngumu kuwa mfuazi wa Kristo. Sio kitu cha siri sana, au fumbo la kufumbua. La kumshukuru Mungu, haitegemei sana uwezo wa kanisa kuieneza injili, pamoja na kwamba baba yetu kwa neema yake ametupatia jukumu katika zoezi la kuieneza injili. Yesu kwa kifupi anasema "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, name nitawapumzisha" (Mathayo 11:28). Hasemi lini, hasemi "Oh, kila mmoja lazima ufanye hivyo kwa muda Fulani au utachomwa."

Mokombozi ameshamaliza kila kitu hadi mwisho. Ni kama ametusaidiwa kwa hila katika hukumu ya mwisho. Mungu hakumtuma mwanae ili amwaminie asipotee bali apate uzima wa milele (Yohana 3:16), hakika hakumtuma tu ulimwenguni ili auhukumu, bali ulimwengu uokolewe kupitia kwake (Fungu 17), na Mungu alimpatia Yesu jukumu la hukumu – umemfanya Yesu kuwa hakimu mkuu katika hukumu ya mwisho.

Huyu sio Mungu tuliyemzoea tangu utotoni, tuliyeelekezwa ni mkatili, anayengojea watu wafanye dhambi kidogo tu ili awatupe kwenye ziwa la moto, anayengojea watu wabahatishe

kutokuwa na dhambi ili awalipe kwa kuwaruhusu kuingi kwenye ufalme. Huyu ni Mungu wa Biblia, anayetoa neema yake kwa kila mtu atakayeikubali.

Mungu anahakikisha hakuna atakayepotea bure. Yesu Kristo anafuatilia kwa karibu kila mmoja aliyewahi kuishi, na amefanya mambo maku kutuhakikishia kila mmoja wetu mahali katika meza ya bwana. Hatalazimisha mtu kuchukua nafasi yake. Vile vile hatamhukumu mtu kwasababu tuliyopewa injili kueneza hatukumfikishia kabla ya kufa kwake. Neema ya Mungu haitegemei uwezo wetu wa kuieneza injili.

Watu wanapofariki wanahukumiwa (Waebrania 9:27). Ni hukumu ya mwisho. Anayekalia kiti cha hukumu si mwingine bali aliyena alama za wokovu wetu, na amini usiamini anayo habari njema! Hutakuta funzo hata moja kwenye Biblia kuwa, pamoja na imani nyingi, kuwa Yesu hana uwezo wa kuokoa mtu hata baada ya kufariki. Kwa maneno ya hitimisho ya musiki wa Les Miserables: “Hata kwa ulimwengu unaopiga mweleka, upo mwale usiozimika, hata usiku uliozidi giza utaisha na hatimaye jua litaangaza.”

Bila kujali alichotaka kumaanisha mwandishi, huu sio msemo tu wa kufurahisha tu. Ni ukweli wa Mungu. Yesu ndiye mwale wa milele, hata usiku uliotanda giza umepata mwisho wake jua la utakatifu limeangaza (Malaki 4:2), kupitia jina pekee chini ya mbingu ambapo kila mmoja anapata uokovu (Matendo ya Mitume 4:12).